

Metafizikia ya Kuwapo katika Methali za Waswahili: Uhakiki wa Kiudenguzi

Issa Y. Mwamzandi

Ikisiri

Metafizikia, kimsingi, ni falsafa inayohusu uchunguzi wa chanzo cha fikra na maarifa kuhusu dhana mbalimbali hususan zile ambazo ni za kidhahania. Katika makala haya metafizikia ya kuwapo ni dhana maalumu inayohusiana na jinsi wanajamii wa Kimagharibi wanavyoapania kuwa na kitovu mahususi ambacho kila kitu kingeibukia. Ni fikra inayohusishwa na mwanaudenguzi Mfaransa Jacques Derrida ambaye anazona jamii hizi ziking'ang'ania kitovu hicho wanachokiona cha thamani na ambacho huenda kikawa Mungu, ukweli, mwanzo, au hata utu. Kitovu hiki kinachoenziwa na kuchukuliwa kuwa adili na wanajamii ndicho Derrida alichokiita *logocentrism* (nenofunge). Makala yanapendekeza kuwa jamii ya Waswahili nayo imejengeka katika fikra kama hii ambapo kila kitu kinawekwa katika kitovu maalumu, na hivyo basi metafizikia yao mahususi ya kuwapo. Makala yanafuatilia mbinu kuu ya kiudenguzi ya kuiweka wazi metafizikia ya kuwapo kwa kuzingatia ukinzani wa jozi za maneno katika methali maalumu za Waswahili. Ili kufikia lengo hilo, makala yamezamia kikoa mahususi cha methali za Waswahili kinachozungumzia ukinzani uliopo kati ya kuwapo/kutokuwapo na kubainisha jinsi metafizikia ya kuwapo, kama ilivyoendelezwa na Derrida, inavyoweza kueleweka. Sampuli ya methali 16 imetumiwa kwa kuzingatia kigezo cha kuzungumziwa ama kuwapo au kutokuwapo kwa sifa fulani. Kikoa hicho cha methali kinahusisha methali zinazoanza na mzizi wa kivumishi '-enye' au zile zinazotaja kuwapo/kutokuwapo moja kwa moja. Hitimisho la makala haya ni kuwa kuwapo, sawa na kutokuwapo, mapenzi/chuki, wazee/vijana, wema/ubaya, wengi/wachache, mafundi/wanafunzi na jozi nyinginezo ambazo mara nyingi hutenganishwa na Waswahili zimebainishwa kama zinazoathiriana na kujengana kimaana – tofauti na fikra yetu kwamba zimeachana kama lilivyo jua na mbingu. Kwa sababu hiyo, methali za Waswahili zimejengeka katika fikra ya kiudenguzi inayohakiki utepetevu wa lugha na kutoimarika kwake kama msingi wa mawasiliano.

1.0 Utangulizi

Nadharia mamboleo za fasihi, hususan zile za baada-umuundo, zimekusanya changamoto za kila aina. Nadharia ya udenguzi ya Mfaransa Jacques Derrida, ambayo ndani yake mnazungumziwa metafizikia ya kuwapo, ni miongoni mwa nadharia ambazo zimehodhi ndani yake mijadala mipevu ya kifalsafa, mbali na istilahi nzito, tena kavu zilizotumiwa humo (Davis, 1992 na Mwamzandi, 2000). Tajiriba yangu kama mwanafunzi na kisha mwalimu wa nadharia za fasihi imenifunza kuwa nadharia hizi zina tabia za kuwatanza hata wasomi waliokomaa. Kwa utaratibu huo, ipo haja ya kuzipatia nadharia hizo fikra na umbo la Kiafrika, likiwemo la Kiswahili, ili mijadala iliyoandikwa humo ifahamike bayana.

2.0 Metafizikia ya Kuwapo katika Mukadha wa Makala

Ni bora tangu awali kuweka bayana metafizikia ya kuwapo/kutokuwapo inayoendelezwa katika makala, hususan ile inayolengwa na methali za Waswahili. Hii ni kwa sababu dhana hii huchukua maana ya kijumla katika Kiswahili, tofauti na ilivyo katika Kiingereza. Kiingereza, kwa mfano, huzungumzia metafizikia ya:

- a) *Existence/Essence*, na
- b) *Presence/Absence*.

Katika jozi zote mbili, Kiswahili hutumia visawe vya kijumla sana vya Kuwapo/Kutokuwapo ingawa kile kinachodhamiriwa katika Kiingereza na jozi hizo mbili ni tofauti sana. Jozi ya kwanza imeendelezwa sana na wanafalsafa wa kidhanaishi kama vile Martin Heidegger na John Sartre ambao wanazungumzia falsafa ya maisha ya binadamu. Hawa wanadai kuwa ‘kuwapo’ yaani *existence*, hutangulia sifa zinazomfafanua na kumtambulisha binadamu au *essence*. Heidegger (1962) anamwita binadamu *Dasein*, yaani kiumbe aliyepo duniani ambaye husukumwa na mifanyiko ya kimaisha kuchagua moja kutokana na mambo anuwai anayopaswa kuyafanyia uteuzi. Sartre (1992) anasema kwamba binadamu lazima ahisi anaishi ndipo mambo mengine yamfungukie katika hali ya kuishi. Wanavyosema, binadamu hujikuta tu katika dunia, yaani huwapo, bila ya kupenda na kuwapo kwake ni tokeo la kifadhi na la muhimu. Ubinadamu wake huja baadaye pale atakapofanya mambo yatakayoyapa maisha yake thamani. Kinyume chake ni binadamu huyu kukosa kuiona thamani ya maisha na kukata tamaa. Inapotokea hivi, wadhanaishi hupatwa na hisia za upweke na uchungu. Utupu huu ndio wanaouona ukiwa sawa na kifo na unaorejelea ‘Kutokuwapo.’

Metafizikia ya pili ya Kuwapo/Kutokuwapo na ambayo imekusudiwa na makala ni ile ya pili inayorejelewa na jozi ya *Presence/Absence*. Hii ni jozi inayoendelezwa na mwanafalsafa Derrida hasa anapotathmini kwa kina metafizikia ya kuwapo kwa kuihusisha na kile kinachopendelewa na wanajamii wa Kimagharibi kama kiini au kitovu kinachotawala fikra zao. Kitovu hiki huwakilisha mambo adili, tena safi na ambayo kila mwanajamii anatarajiwa kujinasibisha nayo. Kinyume na kitovu hiki huwa ni mambo ya kukinaisha, yasiyokuwa na mwelekeo, tena ghushi. Falsafa hii ni tofauti na ile ya kina Nietzsche na Heidegger ambapo ‘kuwapo’ kunahusishwa na kujitambua kwa binadamu na kujifahamu mahala alipo na sifa zake kama kiumbe kilicho hai. ‘Kutokuwapo’ ni sawa na kifo.

3.0 Derrida na Metafizikia ya Kuwapo katika Mfumo wa Lugha

Metafizikia ya kuwapo ni dhana inayorejelewa na waasisi wa kidenguzi kufafanua namna jamii za Kimagharibi zinavyojihusisha na jitihadi za kuinjika kila kitu katika kitovu maalumu. Dhana hii inahusishwa sana na mwanafalsafa wa kidenguzi Jacques Derrida (1930-2005) ambaye mnamo mwaka 1966 aliwasilisha makala yaitwayo '*Structure, Sign and Play in the Discourses of the Human Sciences*' katika Chuo Kikuu cha John Hopkins huko Marekani. Derrida alidhamiria kubainisha kwamba umuundo, ambao ulikuwa umezagaa wakati huo, ulikuwa na dosari nyingi hata baada ya kutupilia mbali kipaumbele alichopewa mwandishi kama kitovu cha maana katika fasihi hadi ikafikia hatua ya baadhi ya wanaumuundo kama vile Barthes kutangaza kifo chake (Webster, 1990). Derrida anahoji kwamba walichofanya wanaumuundo ni kukihamisha kitovu cha maana kutoka kwa mwandishi hadi kwenye lugha. Kwa kufanya hivyo, Derrida aliona kuwa wanaumuundo bado wanazugwa na fikra kongwe ya kuthamini vitovu kama ilivyokuwa tangu jadi. Kung'ang'aniwa kwa kitovu ambacho huonekana kitu cha thamani ndiyo metafizikia ya kuwapo ambayo Derrida anajaribu kuielezea na kufafanua dosari zake. Kitovu hiki, wanavyoeleza wadenguzi, hutumiwa kama msingi wa kuwapo na hivyo basi chombo maalumu cha kudhibiti maana zote zipatikanazo katika jamii za Kimagharibi. Kiini hiki, tangu enzi za kina Plato, kimehodhiwa na vitu kama vile Mungu, nafsi, ukweli, mwanzo, mwisho, urazini na kadhalika (Selden na wenzake, 2005; Carter, 2005).

Derrida anayanyumbua mawazo haya na kuhakiki uwili uliopo katika lugha kama ulivyozungumziwa na mwanaisimu Ferdinand de Saussure. Lugha, anavyosema Derrida, hutenganisha wema/ubaya, nuru/kiza, mrefu/mfupi, mume/mke, ambapo neno la kwanza katika jozi hizi hupendelewa kuliko la pili. Upendeleo huu ndio unaoendeleza metafizikia ya kuwapo kwa kuwa jamii inalifanya neno la kwanza katika jozi kuwa la uhakika, la kweli na lililo adili. Lile la pili linaendeleza dhana ya kutokuwapo na jamii hupania kulinyamazisha na kulihusisha na ughushi. Hata hivyo, Derrida anaona kwamba haya ni mawazo tu ya wanajamii ya kutaka kuwe na utenganisho wa maneno hayo katika jozi. Dhana ya pili huwa haipo tu kiajali na ukweli ni kwamba maneno hayo yanajengana na kamwe hatuwezi kuelewa moja kati ya maneno hayo bila ya kurejelea la pili. Maana katika lugha imejengeka kidenguzi au kiubomozi kwa kuwa 'kuwapo' kwa uzuri kunajengwa na ubaya 'usiokuwapo' kwa wakati huo.

Waswahili, kama wanajamii, nao wana mfumo wao unaowaongoza katika kubuni metafizikia yao ya kuwapo ambayo huenda ikawa tofauti na ile ya

wanajamii wa Kimagharibi. Kwa kuzingatia methali mahususi, makala yanachanganua umbo la kitovu cha wanajamii hawa hasa kwa kuzingatia ukinzani unaoendelezwa na jozi za maneno. Mbali na kuzamia kwa kina ukinzani wa kuwapo/kutokuwapo kama msingi wa kudengua metafizikia ya kuwapo katika jamii ya Waswahili, makala vilevile yamedadisi jozi nyinginezo zilizomo ndani ya methali hizo.

4.0 Misingi ya Kinadharia

Kani ya wanajamii wa Kimagharibi ya kutaka kuandika kila kitu katika kitovu mahususi na ambayo ilitawala fikra zao ndiyo iliyoitwa *logocentrism* au nenofunge. Mwananadharia Derrida katika andiko lake la *Of Grammatology* la mwaka 1976, ameifafanua dhana *logocentrism* ambayo chanzo chake ni dhana *logos* (katika Kigiriki kurejelea ‘neni’) na ambayo katika *Agano Jipya* inaashiria sana kuwapo na ukaribu wa Mungu kwa kuwa Neno la Mungu daima husema: “Hapo mwanzo kulikuwa na neno.” Derrida anaonesha kuwa kuwapo huku ndiko kunakohusishwa na kuwapo kwa nafsi inayozungumza - na neno la Mungu lina athari pevu zaidi kwani lina uzito kuliko neno linaloandikwa (Bertens, 2001). Mwanafalsafa huyu anahitimisha kwa kusema kuwa mfano huu wa neno linalosemwa na Mungu ni kielelezo cha namna neno linavyoweza kufungwa (hivyo basi istilahi nenofunge) na kupata hadhi zaidi kwa kuwa anayesema (Mungu) huwa yupo na kwamba matokeo ya usemi wake ni ya kiyakinifu na yenye uhakika. Pale Mungu anaposema, “Kuwe na mwangaza” matokeo yake ni ya mara moja na papo kwa papo kwani tunaambiwa, “Kukawa na mwangaza.” Haya ni tofauti na maandishi ambayo huhusishwa na kutokuwapo kwa mwandishi ambaye daima huwa hayupo na kamwe hawezi kukitetea kile alichokiandika. Chambilecho Plato katika Schmitz (2007: 116) anayedai kuwa, “Maandishi hayawezi kujitetea na yanamhitaji babake, yaani mwandishi, kuyasaidia”. Aidha, maandishi yanasemwa kuwa yanaweza kusomwa na kutafsiriwa visivyo bila ya uwezekano wa mwandishi kusahihisha kile alichokidhamiria.

Kutokana na usuli huo uliotolewa na Derrida, wadenguzi wamefanya ada kudadisi kile kinachojenga ‘kuwapo’ kwa kukihusisha kile ‘kisichokuwapo’ na kinachobezwa ili kufikia maana kamili ya matini. Kama mbinu ya kiuchanganuzi katika fasihi, wadenguzi hupania kuzibomoa matini au sehemu zake ili kubainisha kutokamilika na kujichanganya kwa matini hiyo. Pale matini inapopania kueleza jambo, wadenguzi hutuhimiza tuangalie kwa umakini kile ambacho matini hukisema bila kutarajia au ikakinyamazisha. Lakini je, ni mambo gani ya kimsingi ambayo tunaweza kuyaangazia katika kuidengua metafizikia ya kuwapo? Kuna mbinu tatu za kidenguzi ambazo zitatusaidia

kuelewa namna Waswahili wanavyoiona metafizikia yao ya ‘kuwapo’, hususan katika methali.

- (i) Mbinu kuu na muhimu inayotumiwa na wanaudenguzi ni ukinzani wa jozi za maneno. Ukinzani huo wa kijozi ni fikra iliyoenziwa na wanaumuundo ingawa wadenguzi hujiona wanaenda hatua mbele zaidi kwa kuona kuwa ukinzani huu huwa wa kihadhi. Tasnifu ya wadenguzi kuhusu jozi hizo ni kuwa jamii za Kimagharibi zimejenga upendeleo wa wazi, tena wa fujo, pale neno moja katika jozi husika linapowakilisha utukufu au kile kinachopaniwa kufikiwa kama kitu adili huku dhana ya pili ya jozi hiyo hiyo ikiangaliwa kama ghushi, isiyo safi na ya daraja la chini. Wanafalsafa wa awali, kama anavyodokeza Derrida, waliuona ulimwengu katika muktadha huo. Waliuona upande wa kwanza wa jozi za maneno kama unaojengwa na vitu vya kimsingi na vinavyostahili kupewa kipaumbele kama vilivyo safi, vya wastani na vilivyokamilika. Upande wa pili wa jozi nao ulifafanuliwa na vitu vilivyotandwa na utata, vyenye doa na umahuluti. Kwa sababu hiyo, usanifu wa hoja katika nchi za Kimagharibi una tabia ya kuviona vitu na hali mbalimbali kwa namna ya upendeleo. Pamoja na mgawo huo ambao wanafalsafa wa kijadi walipania kuujenga, wanaudenguzi hulenga kufutilia mbali mipaka hiyo na kuonesha kuwa jozi za maneno ni mfano wa sarafu moja yenye pande mbili. Udenguzi hubainisha kuwa nuru na kiza ni vitu ambavyo wanafalsafa wa kijadi wangevitenganisha kwa kuipendelea nuru kuliko kiza. Kwa wadenguzi, nuru na kiza vimechangamana na huwezi kukielewa kimoja bila kingine. Hatungeweza kumaliza kile tunachokifahamu kama nuru iwapo lugha tunayoitumia haingekuwa imeratibu ndani yake dhana ya kiza.
- (ii) Udenguzi hushughulikia kwa pamoja jozi za maneno yanayokinzana na wakati huohuo kubainisha itikadi kuu inayojitokeza na inayostahili kusailiwa upya. Kupitia uchanganuzi makini wa lugha katika matini, wadenguzi hudhihirisha ukinzani na utepetevu wa matini hizo. Hili ndilo linalosababisha wadenguzi kudai kuwa, matini hujiumbua na hujibomoa yenyewe na wala sio wao wanaofanya hivyo. Wanavyodai, hii ni sifa ya azali na iliyomo katika lugha kwani tangu jadi lugha imejengeka kama mfumo wenye ukinzani na unaotofautisha maana. Lugha yenyewe imejengeka kiudenguzi kwa kuwa hubainisha tofauti zilizomo ndani yake – za kimaana na za kiitikadi. Hapa ndipo tunapopaswa kuzitafakari methali na ile metafizikia ya kuwapo kwani methali za Waswahili zinajaribu

- kuonesha dosari au na tija ya kuwapo au kutokuwapo katika miktadha mbalimbali inayorejelewa na methali inayohusika.
- (iii) Wadenguzi huenda hatua nyingine mbele na kuonesha kuwa wakati mwingi matini huzungumzia kile isichodhamiria kukisema. Hili hujiri pale matini inapopania kueleza itikadi kuu na maana inayoipendelea na wakati huohuo kujaribu kunyamazisha sauti kinzani na kile isichokipendelea. Kwa mfano, pale mwandishi anapoeleza wazo fulani, njia yake kuu ya kufanya hivyo ni kupitia lugha ambayo, kwa bahati mbaya, imejaa ukinzani usioweza kudhibitiwa hata na mwandishi. Hilo ndilo limesababisha wadenguzi kumnukuu de Saussure akiifafanua lugha kama mfumo wa kutofautisha na kubainisha maana. Kwa utaratibu huo, wadenguzi wanadai kuwa maana ya neno katika lugha huathiriwa na maneno mengine katika lugha hiyo. Kwa sababu hiyo kulielewa neno katika sentensi au usemi kunayashirikisha maneno mengine. Hivyo, maana ya maneno haiwezi kubakia kuwa moja na daima maana ya kitu itagombaniwa na kubadilika kila uchao. Lugha kwa hiyo, kwa wanaudenguzi, haina maarifa razini ya kile inachokizungumzia kwani daima maneno yake hayasanifu hoja zake kwa ukamilifu yakiwa pweke bali inafanya hivyo kwa kutegemea maneno mengine inayohusiana nayo na wakati mwingine yasiyokuwapo. Hatima yake ni kuwa kile kinachosemwa hakiko imara kama tunavyokidhanika kuwa na huwa kinaumbuka kimantiki na kusheheni maana zinazoselea na zinazoahirishwa. Maana hizo huibuliwa na wadenguzi pale wanapozitalii nyufa au mianya inayoachwa na matini. Hatima ya kufanya hivyo ni kutenga au kutoa maana tofauti na ile inayoendelezwa na matini. Matini mbadala huibuka na kuchukua mahala pa matini iliyodhamiriwa hapo awali na mwandishi.

Makala yamefuatilia mtazamo huu wa kiudenguzi na unazitazama methali kama fani iliyojengwa na mfumo huu wa kuwapo. Katika semi hizi, tunapata fikra kuu, tena za asili, ambazo zinatarajiwa ziwe msingi imara wa maongozi kwa wanajamii.

5.0 Udenguzi kama Mbinu ya Kukokotoa Metafizikia ya Kuwapo katika Methali

Makala yamechukua utaratibu maalumu wa kubainisha namna udenguzi unavyoweza kuchukuliwa kama mbinu ya uchanganuzi wa suala la metafizikia ya kuwapo katika methali. Ili kufikia lengo hilo, hatua mahususi zimefuatwa. Hizo ni pamoja na:

- (i) Kuchukua viko vya methali ambazo zinaelekea kupendekeza ‘kuwapo’ kwa dhana maalumu za kimsingi na za adili zinazopendelewa katika methali husika. Mazingatio maalumu yametolewa kwa kikoa mahususi cha methali zinazoanza na vivumishi vyenye mzizi ‘-enye,’ yaani ‘Penye’ na ‘Mwenye’ na ambavyo huashiria ama kuwapo au kutokuwapo kwa sifa fulani pamoja na tija/hasara zinazohusishwa na sifa hizo. Sambamba na kuangazia methali zinazozungumzia kuwapo, makala yameangazia pia methali zinazozungumzia moja kwa moja maneno kuwapo/kutokuwapo au yanayohusiana nayo kietimolojia. Hiki ndicho kikoa mahususi cha methali ambacho makala yanakitumia kuzungumzia metafizikia ya kuwapo.
- (ii) Kubainisha dhana zinazokinzana na ile inayopendekezwa, yaani inayoendeleza kuwapo, na namna inavyoathiri maana ya methali. Tukumbuke kuwa udenguzi hushikilia kuwa mfumo wowote umejengwa na jozi na mipaka inayowekwa huwa ndani ya fikra zetu tu. Kila mara basi, tutazingatia pia kile kinachoonekana kama ghushi na kinachobezwa. Kwa utaratibu huo, tutakuwa tukiendeleza hoja kuwa methali zinafuata msingi huu wa kidenguzi ambapo kinachoelezwa waziwazi kimebeba pia kile kinachonyamazishwa.
- (iii) Kudengua na kuibomoa maana kama inavyotolewa na methali zenyewe. Hapa, sehemu zile zinazojitanza katika methali zitafuatiliwa kwa makini. Makala yametoa mifano mahususi ambapo lugha, kama inavyotumiwa katika methali, inadhihirisha mchanganyiko wa hisia mintarafu ya jozi za maneno. Methali zinauchangamkia na pia kuutosa mgawo wa maneno ambayo Waswahili wameonesha kuwa chanya au hasi.

6.0 Uchanganuzi wa Data

Makala yametumia kanzi ya methali zinazopatikana katika *Kamusi ya Methali* (Wamitila, 2001) ambayo imekusanya zaidi ya methali elfu mbili mia tano. Jumla ya methali kumi na sita (16) zimetumika huku azma kuu ikiwa ni kubainisha ruwaza kuu ya metafizikia ya kuwapo na jinsi inavyoendelezwa ndani ya methali za Waswahili. Data iliyochanganuliwa imefuata utaratibu wa kukidadisi kitovu cha maana na kubainisha utegemezi wake kwa kile kinachochukuliwa kuwa kimelea na kisicho thamani.

6.1 Metafizikia ya Kuwapo katika Methali Zinazoanza na Dhana ya ‘Kuwapo’

‘Kuwapo,’ kama inavyobainishwa na kikoa cha methali zinazoanza na ‘Penye’ au ‘Mwenye’ (ambayo kietimolojia yanahusiana na kuwapo kwa sifa mahususi) ni kitu kinachopendekezwa na kimehusishwa na tija nyingi. Katika *Kamusi* niliyoitumia kukusanya data kuna methali kumi na tano zinazoanza na neno ‘Penye’ huku nyingine thelathini na tano zikianza na ‘Mwenye.’ Baadhi ya methali hizo ni kama vile:

1. Penye **mapenzi** hapapotei
2. Penye **mavi** hapakosi uyoga
3. Penye **nia** pana njia
4. Penye **wazee** haliharibiki neno

Katika methali hizi ni bayana kuwa ‘kuwapo’ ni kitu adili cha kutendwa na mwanajamii hasa tunapotafakari tija zinazoandamana na ‘kuwapo’ huko. Derrida angetuhimiza tufuatilie kile kinachostahiwa na kuwapo ambacho ni mapenzi, mavi, nia na wazee katika methali hizo. Katika methali ya 1, mapenzi ni kitu cha kudumu na daima athari yake hubakia kwa muda mrefu. Methali ya 2 nayo inayapa mavi taswira nzuri ingawa sote tunafahamu kuwa kinyesi si kitu cha kuonewa fahari. Katika muktadha huu, uyoga ni chakula kinachompa mwanadamu siha nzuri ijapokuwa kinategemea kuoza kwa kinyesi ili unawiri. Mavi basi yanakuwa kitu cha tunu hata tunapofahamu karaha yake. Nia nayo (methali ya 3) inapotiwa hutoa ufanisi kwa yule anayetia azma ya kutekeleza jambo hata likiwa na uzito. Hatimaye, methali ya 4 inaelekea kuwastahi wazee na tajiriba yao maishani ni dhamana tosha ya kuiongoa jamii na changamoto inazoikumba.

Ingawa hivyo, maana ya methali bado inaselea kwa kuwa vipo vitu vinavyoachwa na ambavyo vinahitaji kusailiwa zaidi. Hii ndiyo mianya inayozungumziwa na Derrida ambayo huwaelekeza wadenguzi kuona namna lugha (na hapa methali) inavyokaribisha maana mbadala na ambayo inajaribu kuzinyamazisha (Di Yanni, 2000). Ijapokuwa hatujaelezwa kile tunachotahadharishwa kisiwapo, bado tunahisi kuwa ukamilifu wa methali zote nne haupo tu katika methali zenyewe bali umo pia katika maneno yasiyokuwapo. Derrida angedai kuwa maana haijafikia kikomo na hapa imeahirishwa tu na bado ina uwezo wa kupanuka kwa kuzingatia kisichokuwapo (Burman na MacLure, 2005). Hii ndiyo mianya inayoachwa na methali na ambayo tunastahili kuiziba ili tufikie ukamilifu wa maana ya methali hizo. Hivyo basi, tunaweza kuwa na jozi zifuatazo: mapenzi/chuki, mavi/usafi, nia/pasipo na nia, wazee/vijana. Katika mfumo huu, ni dhahiri kuwa neno la kwanza katika jozi ndilo linalopewa kipaumbele katika jamii ya Waswahili na kuonekana adili huku la pili likiwa na doa.

Ili kuthibitisha kuwa jozi hizi zimefungamana, ingawa methali hazijakiri hilo waziwazi, zipo methali ambazo zinayakinisha kupendelewa kwa neno la kwanza katika jozi hizo huku neno la pili likitiliwa shaka. Hapa nitatoa mifano miwili ya methali ambazo zinazungumzia vijana (katika jozi wazee/vijana) na kisha chuki (mapenzi/chuki) ili kukongomea wazo kuwa Waswahili wana upendeleo wao wa kile wanachokiona kama kitovu cha hekima zao.

5. Ngoma ya wana haikeshi
6. Chuki humchoma anayehifadhi

Mifano hii inaweka wazi kuwa wana (vijana) pamoja na chuki ni sifa zinazokaripiwa sana na Waswahili. Katika methali ya 5, vijana wanahusishwa na fujo na uharibifu. Hivyo basi, inakuwa muhali kwao kuendesha mambo yao bila kuzuka kwa takilifu – tofauti na wazee ambao tumeambiwa hawawezi kuliharibu jambo. Chuki (methali ya 6) nayo imetenganishwa na mapenzi na kuoneshwa hapa, kama sumu iliyo na uwezo wa kumfisidi aliyenayo. Imepewa sifa ya moto unaoweza kumchoma mtu kwa kuwa mwenye chuki atakuwa na mafundo moyoni na ambayo hayatamfaidisha kitu ila kumpa shakawa. Shaaban Robert ana methali inayoeleza zaidi sumu hiyo anaposema, “Chuki hupotoa haki na watu” (2007: 11). Chuki hapa inatajwa kama kitu kisichoongoka na ambacho huwafanya watu wasifuate maadili yanayowafaidisha na kuwa msingi wa kuimarisha uongo.

Ili kushadidia hoja kuwa methali huacha nyufa ambazo nimezifuatilia katika methali tofauti hapo juu, tunaweza sasa kuchunguza baadhi ya methali ambazo zinaweka wazi mivutano hiyo ya kijoji katika methali moja. Tazama mifano hii:

7. Penye mafundi hapakosi wanafunzi
8. Penye mbaya wako na mwema wako hakosi

Methali za 7 na 8 zinazungumzia kuwapo kwa jozi mbili zinazokinana, tena kwa wakati mmoja: mafundi/wanafunzi, mbaya/mwema. Katika methali ya 7 mafundi wanaenziwa na wanapewa hadhi kuliko wanafunzi. Hivyo wanapokuwapo inafuatia kwamba wanafunzi sharti nao wawepo. Mafundi na wanafunzi si watu wa kufu moja kama inavyoashiriwa na methali “Cha mkufunzi mwanafunzi akila hufa.” Uwezo hapa umepewa mkufunzi ambaye ana mamlaka juu ya yule anayemfundisha. Ingawa methali ya 8 imetanguliza mbaya na mwema kufuata baadaye, inabainika wazi kuwa mtu mwema ndiye anayeleta matumaini na ndiyo sababu kuwepo kwa mbaya hakuwezi kamwe kukamdhuru mtu kwa kuwa mtu mwema aliyepo mahala hapo anatosha

kumkabili mbaya. Ziko methali kadhaa zinazozungumzia wema kama kitu adili na cha faradhi (Wema hauozi, Wema huzaa wema, Chanda chema huvishwa pete, n.k.) na pia zipo zinazobainisha ubaya kama kitu kisichotamanika (Ubayu hatima yake mbaya, Mwisho wa ubaya ni aibu). Aidha, zipo methali zinazochanganya jozi yote ndani yake na humo wema umependekezwa huku ubaya ukidunishwa (Chema chajiuza kibaya chajitembeza, Mkataa pema pabaya panamwita, n.k.).

6.2 Kutokuwapo na Hasara Zake

‘Kuwapo’ kunakinzana na kutokuwapo na zipo methali zinazobainisha hilo na zinahusisha kutokuwapo na hasara za kila aina. Baadhi ya methali zinazozungumzia kutokuwapo ni pamoja na:

9. Asiyekuwepo na lake halipo
10. Asiyekuwepo machoni na moyoni hayumo
11. Asiyehudhuria ndiye ahukumiwaye

Inakaririwa hapa kuwa kutokuwepo ni sawa na kujivutia mikasa. Methali ya 9 inatoa picha ya kijumla ya lile litakalomsibu asiyekuwepo. Kwa muhtasari, asiyekuwepo hatapata fungu lake stahiki – iwe ni mali, ujira wa kazi, mapenzi au chochote chenye faida kwake. Methali za 10 na 11 zinazungumzia mifano mahususi ya kile atakachokosa mtu asiyekuwapo: Mapenzi na hukumu isiyostahiki. Katika methali ya 10, jicho huona kilichopo na hilo linakuwa na athari ya kuyadhibiti mapenzi ya watu wanaopendana. Kinachoonekana kinatuama moyoni kwani hapo ndipo kilipo kiti cha mapenzi. Kwa Waswahili basi, mapenzi hunawiri pale wapenzi wanapoonana kila mara na hilo huifanya mioyo yao iyakinishe mapenzi yao. Kwa sababu hiyo, asiyekuwapo machoni hujikuta ameachwa kwani macho yataona na kuzoea kile kilichopo, yaani mpenzi mwingine. Methali ya 11 nayo inahusisha kutokuwapo na kupitishwa kwa hukumu zenye dhuluma kwa kuwa asiyekuwapo hana uwezo wa kujitetea. Kuwapo, kama inavyokaririwa hapa, kuna nguvu za kulithibitisha neno linalosemwa kama la kweli na la hakika. Methali ya 11 inaafiki yale yanayotokea mbele ya mahakama ambazo huthamini ushahidi unaotolewa mbele yake. Kutokana na hilo, anayefika mbele ya mahakama atapata haki kwa kuwa atapata wasaa wa kujitetea dhidi ya shutuma zinazomkabili. Asiyekuwapo atapokea hukumu ambayo aghalabu huwa ya kusingiziwa tu. Kwa sababu hiyo, Waswahili huthamini kuwapo.

6.3 Utepetevu wa Lugha katika Methali: Kipi cha Kuwapo/Kutokuwapo?

Ipo miktadha maalumu ambapo lugha hushindwa kudhibiti kile inachokisema na hilo limewapelekea wadenguzi kudai kuwa umuundo umejengwa katika

msingi isiyo thabiti kwa kuwa lugha yenyewe wanayoichukua kama msingi muhimu wa kimuundo si imara kama tunavyoidhania kuwa (Eagleton, 1996). Badala yake, lugha hujizonga na kujichanganya ingawa hilo huwa halisababishi kuvunjika kwa mawasiliano. Miktadha kama hiyo inayoifanya lugha ione kane kushindwa kutoa uamuzi thabiti katika jozi za maneno, ndiyo inayofafanuliwa na wadenguzi kama *aporias* (Burman na MacLure, 2005). Katika muktadha huu, lugha hudhihirisha hisia zote mbili za kukubali na kukinai maneno yote mawili yanayokinzana ndani ya jozi moja. Inapokuwa hivyo, huwa inakuwa vigumu kuamua kipi kitu cha adili kuliko kingine. Hapo ndipo Waswahili wanapoenda hatua moja mbele na kuanza kuzungumzia ‘muktadha’ wa methali ili kutetea wendawazimu uliomo ndani ya lugha yao.

Katika mifano yote ya methali tulizozitoe kuwapo kumejitokeza kama neno la hadhi kuliko la kutokuwapo. Hata hivyo, ipo miktadha maalumu ambayo huonesha kuwa hadhi hizi zinapinduliwa na kuwa kinyume mbele. Kuwapo, sawa na kutokuwapo, kunaweza kusababisha fujo na tafrani za kila aina kama inavyoakisiwa hapa:

12. Penye kuku **wengi** hapamwagwi mtama
13. Penye **wengi** pana mengi

Katika mifano hii dhana ya **wengi** ndiyo inayokinzana na wachache au mmoja na kile kinachochukuliwa kuwa kitu adili ni wachache. Katika muktadha huu, kitu au jambo linalotendwa na wengi linahusishwa na vurugu na kutoongokewa kwa lile linalofanywa. ‘Kuku wengi’ wanaorejelewa katika methali ya 12 wanasimamia uharibifu, kutomakinika na kutositirika kwa siri anayoihifadhi mtu iwapo itasemwa hadharani. Itakuwa vigumu kuelewa nani atakayeweza kuichunga siri hiyo na inaashiriwa kwamba watu wachache au mmoja ndiye anayeweza kuihifadhi siri hiyo. Ujumbe sawa na huo ndio unaopatikana katika methali ya 13 ambapo kila mmoja atakuwa na mtazamo wa kitu kimoja na hivyo kusababisha mfarakano.

Wakati huohuo kuna methali ambazo zinaenda kinyume na kile kinachoendelezwa na methali nyinginezo na hapa ipo mifano:

14. Penye wengi hapaharibiki neno
15. Aliye kando haangukiwi na mti
16. Aliye mbali ufimbo haumfikii

Katika methali ya 14 tunaona kuwa wingi umepewa sifa chanya, tofauti na yale yanayosemwa na methali za 12 na 13. Neno wengi linaonekana kama msingi wa

kuongoa kile ambacho kingeharibika. Huo ndio ujumbe unaojitokeza katika methali nyinginezo (Kidole kimoja hakivunji chawa, Wawili si mmoja) ambapo kuwa pweke katika kuyafanya mambo ni dosari. Watu wanaposhirikiana kuyafanya mambo, basi huwa kunatokea sahali katika utekelezaji wa mambo hayo. Methali ya 15 nayo inawaasa wanajamii wajitahidi wakae kando au wasiwepo pale panapoweza kuzuka fujo. Huo ndio ujumbe uliofumbatwa na methali ya 16. Katika methali hizi, kutokuwapo (kuwa kando au mbali) kuna faida na methali hizi zinatoa fursa ya kuona jinsi lugha inavyojaribu kuyatenganisha maneno yake lakini wakati huo huo kubainisha kuwa utengaji huo si wa kiuashii.

7.0 Hitimisho

Makala yamebainisha jinsi methali za Waswahili zinavyosanifu metafizikia ya kuwapo. Kwa kuzingatia ukinzani wa dhahiri na hata wa siri unaozungumziwa katika methali, makala yameonesha kuwa kile kinachopewa hadhi na cheo, yaani kilichopo, kinategemea sana kile kinachoonekana kuwa cha hadhi ya chini na ghushi, au kisichokuwapo. Aidha, kutegemeana huku kwa kuwapo/kutokuwapo ndiko kunakozifanya baadhi ya methali zitoe taswira ya kukosa uamuzi thabiti wa kipi bora kati ya jozi hii ya maneno.

Marejeo

- Bertens, H. (2001). *Literary Theory*. London: Routledge, Taylor and Francis Group.
- Burman, E. & M. MacLure (2005). "Deconstruction as a Method of Research" katika Somekh, B. na C. Lewin (wah) *Research Methods in the Social Sciences*. New Delhi: Vistaar Publications.
- Carter, D. (2006). *Literary Theory*. Reading: Cox & Wyman.
- Davis, C. (1992). *Criticism and Culture*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Di Yanni, R. (2000). *Poetry: An Introduction*. Boston: McGraw Hill.
- Heidegger, M. (1962). *Being and Time*. Tafsiri ya John Macquarrie na Edward Robinson, New York: Harper and Row.
- Eagleton, T. (1996). *Literary Theory: An Introduction*, 2nd Edition, Mineapolis: University of Minnesota Press.
- Mwamzandi, I.Y. (2000). "Nadharia na Usomi: Vizingiti na Mikabala," katika Kimani Njogu, Kitula King'ei, Clara Momanyi na Paul Musau (wah.) *Kiswahili katika Karne ya Ishirini na Moja*. Cape Town: CASAS.
- Robert, S. (2007). *Mithali na Mifano ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Sarte, J.P. (1992). *Being and Nothingness*. Tafsiri ya Hazel Barnes, New York: Washington Square Press

- Schmitz, T.A. (2007). *Modern Literary Theory and Ancient Texts: An Introduction*. Malden, M.A.: Blackwell Publishing.
- Wamitila, K.W. (2001). *Kamusi ya Methali*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Webster, R. (1990). *Studying Literary Theory*. London: Edward Arnold.

